KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 20, Issue 1

2nd Rabi uth-Thaani 1433

24th Feb, 2012

SHEIKH SULEIMAN BIN ALI KHAMIS AL-MAZRU'I

Na: NDUGU GHALIB BIN YUSUF TAMIM

Nilipokuwa tayari kuchapisha kitabu hichi juu ya Maisha ya Sheikh Al-Amin nikamuonyesha mjombangu Prof. Ali Mazrui, na kumtaka aandike utangulizi wa Maisha ya babaake. Kwa muda mrefu Prof. Mazrui hakupendelea kuandika utangulizi huo kwani alidhani kuwa haitakuwa sawa kwake kuandika utangulizi juu ya maisha ya babaake. Imani yake ni kuwa alijua mambo kidogo sana juu ya maisha ya babaake kwani alipokufa mwaka wa 1947, Prof. Mazrui alikuwa kijana wa miaka kumi na tatu na zaidi kidogo na kwa sababu hii aliona kuwa hakuyajua mengi juu ya maisha ya mzee wake huyu alokuwa kiongozi wa watu na mpendwa wa jamii. Ilinichukua muda mrefu kuweza kumrai akubali ushauri huo. Nilipomtolea copy na kuisoma nakili hiyo ndipo aliporidhika kuandika utangulizi huo. Baada ya kusoma alitoa mashauri kadha juu ya kitabu hichi - yeye ni muandishi shupavu wa miaka mingi na ingawa ni muandishi wa lugha ya Kiengereza lakini juu ya hivyo aliweza kunishauri mambo kadha juu ya kitabu hichi cha Kiswahili. Pengine ningeweza kukiandika kwa lugha ya kimombo walakin kisingewafikia wengi wa wale wanaomjua Sheikh Al-Amin na kumthamini - kwa hivyo nikakusudia kwa lugha alosomesha Sheikh ili watu wake na watu wa Afrika Mashariki wafaidike. Nataraji Insha Allah Mwenye-ezi-Mungu atakijaalia kitabu hichi kiwe kielezo japo kwa uchache juu ya bingwa huyu; kwani kama alivyosema tena mareheum Bw. Maka, Sheikh Al-Amin alikuwa bahari ya kina kikuu. Nami nimejaribu kuzamia katika kina hicho nikatoka na kichache hichi - asaa wengi wakaweza kujua muhtasari wa maisha ya Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui.

Moja katika ushauri wa Prof. Mazrui ni kuwa nimeandika kwa urefu maisha ya Sh. Ali bin Abdalla Mazrui, babaake Sheikh Al-Amin, juu ya kuwa Sheikh Al-Amin alimuona babaake kwa muda mfupi sana. Alipokufa Sh. Ali yeye alikuwa ni mtoto wa miaka minne tu. Likawa jukumu la Sh. Suleiman kumlea, kumsomesha na kumuozesha Sh. Al-Amin. Na sikuandika chochote juu ya mtu ambae ndie muanzilishi na mtayarishi wa Sh. Al-Amin juu ya maisha yake. Vipi nitatia maisha ya Sh. Ali ambaye hakuchangia juu ya maisha matukufu isipokuwa katika kuzaliwa kwake tu, halafu nikaacha kutaja maisha ya mtu ambae ndio shina la maisha ya Sheikh Al-Amin - mtu ambae ndiye alokuwa na athari kubwa zaidi juu ya maisha yake. Kwa hivyo Prof Mazrui akaonelea nitakuwa nimefanya dhulma kama sitaandika chochote juu ya maisha ya Sh. Suleiman. Shauri zuri sana.

Juu ya uzuri wa shauri huu wa Prof Mazrui ambao niliwafikiana nao,walakin ulinirudisha nyuma kwa muda wa miaka miwili katika uchapishaji wa maisha hayo, kwani sikuwa nimekusanya chochote juu ya Sheikh Suleiman. Kazi ya ukusanyaji si kazi ndogo kwani nilishaipitia nilipokuwa nakusanya kidogo hapa na kidogo pale juu ya maisha ya Sheikh Al-Amin. Kurudi tena nianze kukusanya juu ya maisha ya Sh. Suleiman niliona ni kazi ngumu sana kwa sababu wengi kati ya wale nilowahoji juu ya maisha ya Sh. Al-Amin walikuwa watu wa nje. Kwani kama ilivyo kawaida utukufu, ushujaa na ubora wa mtu hujulikana nje. Watu wako huwa hawaujui sana utukufu wako wala ushujaa wako wala ubora wako. Kwa hivyo ilinibidi kusafiri baina ya Mombasa na Nairobi, Takaungu, Nyeri na kila niliposikia naweza kupata kitu juu ya maisha ya shujaa huyu. Prof Mazrui kwa hivyo akanipa kazi nyengine ngumu zaidi. Siku zote nikijuta kwa nini sikuanza utafiti wa kitabu hichi wakati wa uhai wa mamaangu kwani yeye alikuwa na mengi sana aloyapata kwa babaake huyu. Walakin majuto ni mjukuu. Ingawa niliwahi kupata kidogo kutoka kwa mamaangu, Bi Aisha Al-Amin Mazrui, na kwa bibi yangu, Bi Swafiya binti Suleiman, mke wa Sh. Al-Amin.

Wakati wa mauti ya Sh. Ali bin Abdalla alimwita Sh. Suleiman bin Ali bin Khamis Mazrui ambaye ni binami yake na mwanafunzi wake na mrithi wake wa elimu, na kumuusia hivi, "nakupa mwanangu huyu (Al-Amin) leo duniani unipe mwenyewe kesho akhera." Subbana Llah! Jukumu zito, kwani mcha Mngu aalim amuusia mcha Mngu, aalim mwenziwe amtizamie mwanawe wa miaka mine hapa ulimwenguni amlee kama alivyokuwa ammi, baba na mababu walomtangulia. Jukumu zito kwani hidaya yatoka kwa Mwenye-ezi-Mngu. Jawabu la Sheikh Suleiman likawa "Insha-Allah." Na kweli masha-Allah Mwenye-ezi-Mngu akamjaza mahaba ya kumpenda binammi yake huyo wa miaka mine na kumlea kwa kite na tamasha, akamfanya ni mwanawe wa kwanza na wa mwisho; akamlea kama alivyowalea wanawe zaidi, kwani Sheikh Al-Amin alilelewa kidhati ya dini akapewa kila elimu alokuwa nayo Sh. Suleiman na zaidi. Alimtanguliza kwa kila kitu kiasi ambacho Sh. Suleiman akiwa katika mitwalaa yake anae Sh. Al-Amin; akiwa katika swala zake za tahajjud, anae Sh. Al-Amin; akiwa katika mahkama yake anae; ikawa unapomuona Sh. Suleiman basi ubavuni mwake yupo Sh. Al Amin. Akamsomesha na kumfundisha adabu, elimu, hekima, heshima, vazi, dini na duniya. Akakolea Sh. Al-Amin kwa kila alichokuwa nacho Sh. Suleiman. Alipokuwa hana cha zaidi

YALIYOMO

SHEIKH SULEIMAN 1 - 3

NE'MA YA KUTAMKA 3 - 4

katika elimu na hekima akawa tayari kumpeleka popote atakapopata cha ziada. Naam! Sheikh Al-Amin akapelekwa Unguja kwa Sayyid Ahmad bin Sumeyt na kwa Sh. Abdalla Abubakar Bakathir, mabingwa na wasomi wakubwa wa Unguja wakati huo. Sayyid Ahmad juu ya kuwa alikuwa aalim mkubwa wa dini vile vile alikuwa baharia mkubwa na nahodha hodari wa meli. Unahodha wa kuaminika ikawa hata anaposafiri utuuzimani mwake basi manahodha wa meli hiyo hawaridhiki kama hajaingia katika chumba chao na kuiendesha meli hiyo. Hao ndio walokuwa walimu wa Sh. Al-Amin, bahari juu ya bahari, elimu juu ya elimu. Huyo Sh.Suleiman ndiye alokuwa mlezi wa Sh.Al-Amin alomukhitari Sh.Ali bin Abdallah kuwa mlezi wa mwanawe.Masha - Allah mlezi bora kabisa.Mwenye — ezi- Mngu awe radhi nao — Amin. Kwa hivyo haya yafuatayo ndiyo machache niloweza kupata juu ya mlezi huyu.

KUZALIWA KWA SH. SULEIMAN NA MAISHA YAKE

Sheikh Suleiman alizaliwa katika mji wa Mombasa, Sh. Suleiman ni mwanafunzi wa Sh. Au bin Abdalla bin Nafy Mazrui ambae kwa kizazi ni bin ammi yake. Yeye ndie alokuwa mrithi wa Sh. Au kwa elimu na mambo yake yote. Katika jumla ya urathi aloupata kwa Sh. Ali ni vitabu vyake, na kikubwa katika hivyo ni Tafsiri ya Jalaleyn aloiandika mwenyewe Sh. Ali kumuandikia babaake ili ende akasomee wakati wa safari yake kwenda masomoni Makka mwaka wa 1937.

Mausio makubwa aloyapata Sh. Suleiman kutoka kwa Sh. Alii ni kukabidhiwa mtoto wake, kwa mausio ya kuwa anamkabidhi mwanawe hapa duniani na amrudishie mwenyewe kesho akhera. Kama alivyokuwa Sh. Ali kuwa ni mlezi hodari alolea mwana mpaka akawa a'alim na Sheikh na mchaji Mngu mkubwa, vile vile na yeye Sh. Suleiman akatumia malezi aloyapata kwa bin ammi yake pamoja na mausio yake nae akamlea Sh. Al-Amin kuwa mwana mwema aalim na Sheikh na mchaji Mngu mkubwa. Malezi mema, mazao mema. Al- hamdu Lillahi.

Kwa hivyo Sh. Suleiman akakulia katika mazingira ya uchaji Mngu na elimu na siasa na heka heka za vita vya Mazrui na Seyyid Said, ushindani wa kidini baina ya miezi wake na Sh. Muhammad bin Au Al-Mandhry alokuwa mufti wa ki-Ibadhi wakati wa ufalme wa Seyyid Maj id (1856-1870) na Seyyid Barghash (1870-1888). Alipokufa bin ammi/mwalimu wake 1894 Sh. Suleiman tayari alikuwa ameshakuwa bahari wa dini, aalim mkubwa. Nae kama alivyokuwa mwalimu wake nae vile vile alipigana vita kuondoa bid-a na itikadi za kiswahili zilopingana na mafund isho ya dini. Hakukubali itikadi hizo zitiwe katika dm1. Vita hivi alipambana navyo vilivyo akisaidiwa na mwanawe ambae pia ni mwanafunzi wake, Sh. Al-Al-Amin.

Katika mwaka wa 1898 Gavana wa Afrika Mashariki, Arthur Hardinge alianzisha mipango ya daraja za mahakama. Kwa hivyo mufti wakati huo akapewa jina la Sheikh-ul-Islam.

Upinzani wa Sh. Suleiman dhidi ya itikadi za kiswahili kutiwa katika U-Islam uliwachukiza wengi khasa wale Mashekhe waloyapenda mambo ya dhikiri, talqini, maulidi na ngoma. Katika mwaka wa l902 jamaa walipeleka ujumbe serikalini kumtaka Mkuu wa Wilaya amchague Mswahili katika cheo cha Sheikh-ul-Islam ambae ndie atakae kuwa Kadhi Mkuu wa Kenya. Kwa vile Waengereza walipenda kuwagawanya watu, walipata fursa nzuri kupalilia vita hivi vya kidini baina ya wale waloshikilia mikazo ya kidini na wale waloyapenda mambo ya bid-a na ngoma za mji. Kwa hivyo kwa ushirikiano baina ya serikali ya Kiengereza pamoja na Liwali Salim bin Khalfan Al-Busaidy, walielemea upande mmoja na akachaguliwa Seyyid Abdur-Rahman bin Ahmad As-Saggaf kuwa Sheikh-ul-Islam na Kadhi Mkuu. Seyyid Abdur-Rahman alijulikana zaidi kwa jina la Mwinyi Abudi au Sheikh-ul-Islam. Sh. Suleiman nae akawa ndio Kadhi wa Mombasa mpaka mwaka wa 1910.

Mwaka wa 1910 Sheikh Suleiman akachaguliwa kuwa Kadhi Mkuu na akashikilia kazi yake hii mpaka wakati alipokufa 1931. Wakati ni alipochaguliwa kuwa Kadhi Mkuu, Sh. Al-Amin alitakiwa achukue nafasi ya Ukadhi wa Mombasa Sh. Al-Amin ambae wakatj huo alikuwa amejishughulisha juu ya kusomesha dini pamoja na uchapishaji wa gazeti hike In Al-Islah, mwanzo alikataa kushika kazi hii ya Ukadhi kwani aliona atakapo shika kazi hii itakuwa vigumu kwake kuendelea na jihadi alojitolea. Sheikh Suleiman akamuomba mwanawe huyu akubali kuichukua kazi hiyo ya Ukadhi kwa kumnasihi kuwa ikiwa ataikataa huenda akachaguliwa mtu amabaye hafai katika kazi hiyo, ikawa yeye ndiye aliyekuwa sababu kubwa ya Sh. Al-Amin kukubali kushika kazi ya Ukadhi. Mwenye-ezi-Mngu ambariki kwa nasaha hiyo – Amin.

MKE NA WATOTO WA SHEIKH SULEIMAN

Kwa hakika Sh. Suleiman aliowa mke mmoja tu nae ni Bi Maryarn binti Muhammad A1-Mazrui. Mwenye-ezi-Mngu akawabariki na kuzaa watoto saba. Naoni:

Sh. Maamun bin Suleiman Mazrui - alowahi kuwa Kadhi wa Mombasa 1932 -1937. Nae akajaaliwa kukieñdeleza kizazi cha Sh. Suleiman kwa kupata watoto sita:

a) Bw. Aziz bin Maamun Mazrui
b) Bi Fureya binti Maamun Mazrui
c) Bi Ramla binti Maamun Mazrui
d) Bi Khànaa binti Maamun Mazrui
e) Bi Huda binti Maamun Mazrui
f) Bw. Mahir bin maamun mazrui

Bi Swafia binti Suleiman Mazrui (Ma-Bilee). Huyu aliozwa Sh. Al-Amin bin Ali Mazrui nao Mwenye-ezi-Mngu akawabariki kuendeleza kizazi cha Sh. Ali bin Abdalla Mazrui na vile vile kizazi cha Sh Suleiman bin Ali Mazrui. Wakabarikiwa kuzaa watoto watano:

a) Muhammad bin Al-Amin Mazrui (alikufa. uchangani)
b) Bi Salma binti Al-Amin Mazrui
c) Bi Nafisa binti Al-Amin Mazrui
d) Bi Aisha binti Al-Amin Mazrui
e) Bw. Au bin Al-Amin Mazrui (Prof. Au Mazrui)

Bi Rafiya binti Suleiman Mazrui (Ma-Dada). Nae Vile vile akakiendeleza kizazi cha Sh. Suleiman kwa kuzaa watoto wane:

a) Bi Sharifa binti Shariff Abdalla Salim (Mama Ifa)
b) Bi Fatma binti Shariff Abdalla Salim
c) Bi Mzamilu binti Shariff Abdalla Salim
d) Bw. Salim bin Shariff Abdalla Salim (Sal Davis)

Bi Saadiye binti Suleiman Mazrui (Ma-Juu). Nae akakiendeleza kizazi cha Sh. Suleiman kwa kupata watoto wawili:

a) Bi Riziki binti Nassir Said Al-Mandhry
b) Bi Khadija binti Nassir Said A1-Mandhry

5. Bi Rehema binti Suleiman Mazrui

(Mama-Ema). Huyu Mwenye-eziMngu alimjaalia watoto wa tatu:

a) Bi Buthaina binti Hemed Salim Mazrui
b) Bi Salma binti Hemed Salim Mazrui
c) Bi Rukiya binti Hemed Salim Mazrui.

6. Bi Shuwena binti Suleiman Mazrui (Bibi Ena). Mwenyezi-ez-Mngu alimbariki watoto wanane:

a) Bi Samira binti (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
b) Bi Khalida binti (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
c) Bw. Shafiq bin (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
d) Bw. Rafy bin (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
e) Bi Asma binti (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
f) Bw. Swaleh bin (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
g) Bw. Abdul-Nassir bin (Maalim) Abdalla Salim Shikelly
h) Bw. Munjid bin (Maalim)Abdalla Salim Shikelly.

7. Bw. Muhammad Suleirnan Mazrui (Abu Suleiman). Mwenye-ezi-Mngu amembariki watoto kumi na moja:

a) Bw. Suleiman bin Muhammad Suleiman Mazrui
b) Bi Sulafa binti Muhammad Suleiman Mazrui
c) Bi Sirini binti Muhammad Suleiman Mazrui
d) Bw. Abdalla bin Muhammad Suleiman Mazrui (Babdala)
e) Bw. Seif bin Muhammad Suleiman Mazrui
f) Bi Sulaima binti Muhammad Suleiman Mazrui
g) Bi Saada binti Muhammad Suleiman Mazrui
h) Bi Sharifa binti Muhammad Suleiman Mazrui
i) Bw. Salim bin Muhammad Suleiman Mazrui
j) Bw. Soud bin Muhammad Suleiman Mazrui
k) Bi Sulaika binti Muhammad Suleiman Mazrui

KUUGUA NA KUFA KWA SH. SULEIMAN

Mwaka wa 1931 Sh. Suleiman alipata maradhi ambayo pamoja na utu uzima alokuwa nao ndio ulokuwa mwisho wa maisha yake. Mwaka huu Sh. Al-Amin ambaye ndie mwana mlezi na mwanafunzi mkubwa wa Sh. Suleiman aliazimia safari ya hija. Kwa kumuona mlezi wake hali alokuwa akataka kuivunja safari ili amuhudumie mzee wake mpaka amukhatimishe Sh. Suleiman kwa kujua umuhimu wa safari ya hija hakukubali mwanawe huyo kuivunja safari ya ibada ya kutekeleza nguzo ya tano ya U-Islam kwani hakuona kuwa ugonjwa wake na hata mauti yake kuwa ni sababu ya kumzuilia mwanawe kipenzi chake kutimiza wajibu wake wa Hija. Alijuwa kuwa binadamu hawezi kutabiri siku ya kufa kwake, wala ugonjwa wake na uzima wa Sh. Al-Amin hauwezi kutabirika ni nani kati yao anaweza kutangulia kufa. Na vile alikhofia khatari ya kucheleweshe au kuakhirisha safari hii ya hija ambayo mtu huenda kwa kulinganiwa na Mwenye-ezi-Mngu peke yake. Kwa hivyo Sh. Suleiman akampa ruhusa Sh. Al-Amin akaitimize amali yake hii ya hija.

Kwa kumuhurumia mlezi wake huyu, Sh. Al-Amin hakutosheka kuondoka tu bila ya kuacha mipango kamili na kumuachia mlezi wake mtu alokuwa na imani nae ili aweze kumuuguza na kumuhudumia. Kwa hivyo Sh. Al-Amin akamuomba Sh. Suleiman amuachie rafiki yake mkubwa wa dhati kuwa badali yake kwa muda huo wa safari yake. Sh. Suleiman alipokubali ndio Sh. Al-Amin akamuandikia barua swahib yake waloshibana (wa chanda na pete), Sh. Abubakar Abdalla Bakathir, aje amuuguze Sh. Suleiman mpaka khatima yake au mpaka atakaporudi kutoka Hija. Sh. Abubakar kwa mapenzi ya swahibu wake ambaye pia ni mwanafunzi mwenziwe walosoma pamoja kwa babaake - Sh. Abdalla Bakathir, bila ya kurudi nyuma wala kusita akachukua jukumu hilo la kumuuguza Sh. Suleiman. Haikupata muda mrefu baada ya kuondoka Sh. Al-Amin huku nyuma Sh. Suleiman akazidiwa na maradhi na Mwenye-ezi-Mngu akaichukua roho ya kiumbe chake kipenzi huku akiwa amezungukwa na wanawe pamoja na Sh. Abubakar (*Inna Lillahi wa Inna Ilaihi Rajiuun*). Hii ndiyo khatima ya mwanaadamu. Sh. Suleiman akazikwa makaburi ya Mazrui ubavuni mwa Sh. Ali bin Abdalla Mazrui.

Ne'ema Ya Kutamka Na Kubainisha

Ne'ema za Allaah juu ya waja wake ni nyingi, nawala hazihisabiki. Na miongoni mwa Ne'ema hizo kubwa ni [ufasaha wa] kuzungumza ambako mtu hubainisha niya yake, na kuweka wazi lengo lake, na kuamrisha mema na kukataza maovu. Na yule ambae atakaeikosa Ne'ema kama hii hatoweza kuyapata mambo kama haya. Na wala haimkiniki kwake yeye kufahamiana na wengine isipokuwa kwa ishara au kwa kuandika iwapo yeye ni muandishi. Amesema Allaah (عزَّ وجلَّ) **"Na Allaah anapiga mfano wa watu wawili (wengine). Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo juu ya bwana wake, popote amwelekezapo haleti kheri. Je! huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu, naye yuko juu ya njia iliyonyooka?"**

Katika tafsiri ya aya hii, imesemwa, "Kwa hakika, huwo ni mfano ambao Allaah amejipigia nafsi Yake na yale masanamu." Na imesemwa, "huwo ni mfano wa *Kaafir* na *Mu'min*." Amesema al-Qurtubee (9/149): "Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas, nayo ni riwaya iliyo *Hasan*, kwa sababu hiyo ni aya yenye kukusanya." Na iko wazi katika kuonyesha upungufu wa mja aliye bubu ambae hafaidishi mtu yoyote, wala hamfaidishi bwana wake kwa njia yoyote anavyomuelekeza. Na akasema Allaah (عزَّ وجلَّ) "Basi naapa kwa Muumba wa mbingu na ardhi hapana shaka (muliyoahidiwa ya kufufuliwa na malipo) ni kweli, kama hapana shaka munavyotamka."

Allaah (عزَّ وجلَّ) ameapa kwa Nafsi Yake juu ya uhakika wa kufufuliwa na kulipwa kutokamana na amali [watakazofanya waja]; kama ambavyo mazungumzo ya ufasaha yanavyoendelea kutokea kwa wale tuwazungumzao. Na katika hayo kuna sifa za hali ya juu katika rehma za ufasaha.

Na akasema (سبحانه وتعالى):"Amemuumba binadamu, akamfundisha kunena."

Al-Hasan akalifasiri tamshi hilo la " al-Bayaan - kunena" kuwa ni mazungumzo [kwa ufasaha]; na katika hayo ni kuzitaja Ne'ema za mazungumzo [kwa ufasaha] ambayo ufahamishaji wa mtu unapoleta sura ya kueleweka katika aliyoyakusudia kuyasema.Na akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Je! Hatukumpa macho mawili? Na ulimi na midomo miwili?"**

Akasema Ibn Katheer katika tafseer yake. Na maneno yake (سبحانه وتعالى) "**Je! Hatukumpa macho mawili?"** Maana yake ni kwamba aone kwayo. **"Na ulimi"** Maana yake ni kwamba autumie kuzungumzia, ili ueleze yaliyomo ndani yake. **"na midomo miwili"** Atafute msaada kutokamana nayo kwa kuzungumza, kula chakula, na kwa pambo la uso wake na mdomo.

Na ni katika [ukweli] ujulikanao yakwamba; neéma hii inakuwa ni neéma ki-hakika iwapo mazungumzo [yenye ufasaha] yatatumiwa kwa yaliyo mazuri.

Amma yatumiwapo kwa mambo maovu, basi hiyo ni laana kwa mwenye kuyatumia hivyo na yoyote aliyenyimwa neéma hii, basi atakuwa kwenye hali iliyo bora kuliko yule ambae alipewa neéma hiyo na akaitumia vibaya.

Kuuhifadhi Ulimi Kutokamana Na Maneno Isipokuwa Katika [Maneno Ya] Kheri

Amesema Allaah (عزَّ وجلَّ): "Enyi mlioamini! Mcheni Allaah na semeni maneno ya sawa (yenye kumfurahisha Allaah). Atawaafikia mfanye mambo mema na kuwasamehe madhambi yenu na anayemtii Allaah na Mtume wake hakika ameshinda ushindi mkubwa." Akasema Allaah (عزَّ وجلَّ): "Enyi mlioamini! Jiepusheni na wingi wa dhana, hapana shaka baadhi ya dhana ni madhambi; musifanyiane upelelezi na wala musisengenyane je yuwapenda mmoja wenu kuila nyama ya mfu wa nduguye? Mukachukizwa. Na mcheni Allaah hapana shaka Allaah ni mwenye kuzikubali toba, mwingi wa kurehemu."

Akaseama Allaah (سبحانه وتعالى): "Na Wallaahi hakika tulimuumba mwanaadamu na tunakijua kinachompitia katika nafsi yake. Na, ilhali sisi tuko karibu zaidi kwake yeye (mwana-adamu) kuliko mshipa wake wa shingo. Pindi wanapokutana wenye kukutana wawili (Malaika wawili) kwa upande wa kulia na upande wa kushoto wenye kukaa. Halitamki neno (mwana-adamu) ila wapo mbele yake Raqeeb na 'Ateed (Malaika wawili wanaandika anayoyasema mwana-adamu na anayoyafanya)". Akaseama Allaah (سبحانه وتعالى): "Na ambao huwaudhi Waislamu, wanaume na wanawake kwa mambo ambayo hawakuyafanya, basi hakika wamezibebesha nafsi zao uongo na madhambi yaliyo wazi."

Na imepokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwauliza Maswahaba zake (رضي الله عنهم): "Nyinyi mwajua maana ya *Gheebah*?" Wakasema, "Allaah na Mtume wake ndiwo wajuao". Mtume (صلى الله عليه وسلم) Akawaambia: "Ni kumtaja ndugu yako kwa jambo lenye kumkirihisha." Wakasema Maswahaba, "je waonaje iwapo ndugu yangu huyo analo hilo nilomsema nalo."Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Iwapo atakuwa analo lile ulomsema nalo, utakuwa umemsengenya, na ikiwa hana lile ulomsema nalo utakuwa umemzulia."

Amesema Allaah (عزَّ وجلَّ) "Na wala usiyafuate usiyoyajua, na yasiyokuwa na faida yoyote. Hapana shaka, msikizi, macho na moyo, yote kwa yaliyoyachuma ni yenye kuulizwa."

Na imepokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Hakika Allaah anaridhia kutoka kwenu [mambo] matatu na anachukia kutoka kwenu [mambo] matatu. Amewaridhia yakwamba mumuabudu Yeye Peke yake, wala musimshirikishe na kitu chochote, na kwamba nyote mushikamane na kamba ya Allaah wala musifarikiane. Na anachukizwa kutoka kwenu mambo ya 'imesemwa' na 'yasemekana', kuuliza masuali mengi na kufuja mali."

Imepokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Mwana-adamu ameandikiwa fungu lake la uzinifu, na hilo litampata hapa budi. Kwa hakika uzinifu wa macho mawili ni kutazama; uzinifu wa masikio mawili ni kusikiya; uzinifu wa ulimi ni kutamka; uzinifu wa mkono ni kugusa; uzinifu wa mguu ni hatua; na moyo hutamani na kupenda, na yenye kusadikisha yote hayo na kukadhibisha ni tupu yake."

Katika swaheeh yake (No. 10), Imaam al-Bukhaari amepokea kutoka kwa 'Abdullaah bin 'Amr (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: "Muislamu [wa kweli] ni yule ambae Waislamu [wengine] wamesalimika na ulimi wake na mikono yake." Amesema al-Haafidh [Ibn Hajar al-'Asqalaani] katika kusherehesha hadeeth hiyo: Hadeeth hiyo ni ya ujumla kuhusiana na ulimi pasi na kuwepo mikono kwa sababu [kwa kutumia] ulimi, pana uwezekano wa matamshi kuwahusu waliotangulia, na wale waliopo katika wakati huo, na pia watakaokuja baadae, kinyume na mikono. Naam! Pana uwezekano yakwamba ushirika wa ulimi unapatikana hapo kwa kuandika. Na kwa hakika, athari yake katika hilo ni kubwa. Na kwa maana hii, utenzi unasema: Nimeandika na nimeiyakinisha siku nilipoandika, Kwa sababu mikono yangu itamalizika na maandishi yake yatabaki. Kwahiyo, Iwapo nilitenda wema nitalipwa mfano wake. Na iwapo nilitenda uovu, basi juu yangu ni hisabu yake.

Katika swaheeh yake (No. 6474), al-Bukhaari amepokea kutoka kwa Sahl bin Sa'd (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyesema: "Ni nani atakaenichukulia dhamana kwa kile kilichoko baina ya ndevu zake na kwa kile kilichoko baina ya miguu yake, na mimi nitamchukulia dhamana ya pepo." Makusudio ya kilichoko baina ya ndevu na miguu ni ulimi na tupu. Katika swaheeh zao, al-Bukhaari (No. 6475) na Muslim (No. 74) [Imepokewa] kutoka kwa Abu Hurairah kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyesema: "Mwenye kumuamini Allaah na Siku ya mwisho, basi na aseme maneno ya kheri au anyamaze." [Mpaka mwisho wa] hadeeth. Katika Shar'h al -Arba'in, kuhusu sherhe ya hadeeth hii, amesema Imaam an-Nawawee: Amesema ash-Shaafiée, "Maana ya hadeeth ni pale mtu anapotaka kuzungumza, basi kwanza na atafakari. Kwahiyo, ikiwa itamdhihirikia yakwamba hapana madhara juu yake, anaweza kuzungumza. Na ikiwa itamdhihirikia yakwamba pana madhara na shaka, basi na ajizuiye." Na ikanukuliwa kutoka kwa baadhi yao yakwamba alisema, "Lau kama ungelikuwa uwanunulie makaratasi wale *mahafadhah*, basi kwa hakika utanyamaza katika mazungumzo mengi." Katika ukurasa wa 45 wa kitabu chake, *Rawdhatu al-'Uqalaa wa Nuzahatu al-Fudhalaa',* Imaam Abu Haatim bin Hibbaan al-Bustee amesema: "Waajib wa mtu mwenye akili ni kujilazimisha kunyamaza mpaka uzungumzaji uwe ni muhimu kwake. Kwani ni wengi wangapi waliojuta baada ya kuzungumza na ni wachache wangapi waliojuta waliponyamaza. Watakaorefushiwa adhabu zaidi katika watu na wakubwa wao watakaofikiwa na balaa za kujaribiwa ni wale waliopewa ulimi wa porojo na moyo ulofungwa. Katika ukurasa wa 47, vilevile alisema, "Ni waajib kwa mwenye akili awe na uadilifu katika masikio yake, na ajue yakwamba yeye ameja'aliwa kuwa na masikio mawili na mdomo mmoja ili asikilize sana kuliko kusema kwa sababu huwenda anapozungumza akajuta, na lau hatozungumza basi hana haja ya kujuta. Nae atakuwa na uwezo wa kumrudi yule mtu, maadamu yeye hajazungumza, atakuwa na uwezo zaidi wa kumrudi yule aliyezungumza. Na atakapolizungumza neno atalimiliki, na iwapo hakuzungumza itakuwa ni kheri." Katika ukurasa wa 49, vilevile alisema, "Ulimi wa [mtu] mwenye akili uko nyuma ya moyo wake. Kwahiyo, anapoazimia kuzungumza, hurudi kwenye moyo wake. Ikiwa lilikuwa ni lenye kumuhusu, yeye huzungumza, na lau kama si hivyo, basi hunyamaza. Mtu mjinga, moyo wake uko kwenye ncha ya ulimi wake; chochote kijacho juu ya ulimi wake hukizungumzia. Mkosefu wa akili katika dini yake ni yule ambae hakuuhifadhi ulimi wake.